# FOMU YA MKATABA WA UJENZI

## A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | MWAJIRI | Mkurugenzi wa Kanda<br>VETA KANDA YA KATI.<br>S. L. P 2084<br>Dodoma – Tanzania |
| 2 | JINA NA ANWANI YA FUNDI MKUU (*Mwajiriwa*) | Jina: JOHN. KISUDA. KISESE<br>Anwani: . MANYARA . . .<br>Simu: . . . 0682 663 475 or 0658 809773<br>Account number 0721740032 79 |
| 3 | ENEO LA UJENZI | IKUNGI -DVTC HOSTEL YA WASICHANA, HOSTEL YA WAVULANA NA GENERAL STORE |
| 4 | MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI | KUFANYA KAZI YA RANGI KUANZIA KUSIKIMU HADI KUKAMILISHA |
| 5 | GHARAMA YA UFUNDI | TSH: 6,200,000/- |
| 6 | MUDA WA MKATABA<br>(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusaini . 29/06/2022<br>Muda: . . 27 . . . (*Siku*)<br>Tarehe ya Kuanza Kazi . 29/06/2022<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi . 26/07/2022 |
| 7 | MASHARTI YA MALIPO: | • Hakuna Malipo ya Awali<br>• Fundi atalipwa kwa awamu . 3 . . baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa |

Scanned with CamScanner

## MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kama mchaganga,kokoto,nondo,cement,mbao,marine n.k kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Fundi mkuu atalazimika kuja na vifaa vyake vya kifundi na usalama eneo lake la kazi kama; refrector,panga,sururu,chepe,ndoo,jembe,safety boot,kofia ngumu n.k
3. Fundi mkuu atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi mkuu asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi mkuu atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi mkuu kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi mkuu atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi mkuu kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Fundi mkuu ahakikishe anamafundi wasaidizi wasiopungua....23.....kila siku
11. Ucheleweshaji wa Kazi:
    - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

Scanned with CamScanner

12. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*. Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

13. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi mkuu au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.
- Mkataba utavunjwa endapo fundi mkuu atashindwa kuajiiri mafundi wasaidizi kulingana na ukubwa wa kazi,kama itakavyoelekezwa na washauri,ama kamati.
- Mkataba utavunjwa endapo fundi hatazingatia nidhamu ya kazi,atasababisha vurugu , taharuki ,migomo ama ugomvi eneo la kazi.
- Mkataba utavunjwa endapo 80% ya mafundi wasaidizi hawatakuwa na Imani na fundi mkuu.

14. Hakutakuwa na ongezeko la gharama zitakazotokana na ongezeko la muda wa mkataba.

**MWAJIRI:**

Saini: [signature] ...........................

Jina : John R. Kawanja ...........................

Cheo: R.D ...........................

Tarehe: 29/06/2022 ...........................

**FUNDI/KIBARUA**

Saini: [signature] ...........................

Jina: JOHN K. KISIGE

Cheo: FUNDI RANGI

Tarehe: ~~29/6/2~~ 29/06/2022

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: [signature] ...........................

Jina: JOHN THOMAS

Cheo: MSIMAMIZI ...........................

Tarehe: 29/06/2022

**SHAHIDI WA FUNDI /KIBARUA**

Saini: [signature] ...........................

Jina: DAUDI ZAKAYO

Cheo: FUNDI ...........................

Tarehe: 29/06/2022 ...........................

Scanned with CamScanner